JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS ,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
**KIWELE SEKONDARI**

S. L. P 733,
**IRINGA**.
TAREHE 30/04/2022

Kumb. Na KWSS/AD/VOL. I/07
Ndugu: …………………………..
S. L. P. …………………………..

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIWELE WILAYA YA IRINGA (V) KIDATO CHA TANO- 2022.**

Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na shule yetu. kuchaguliwa kwako kumezingatia mafanikio uliyo yapata katika kumaliza elimu ya kidato cha nne.

Shule yetu itafunguliwa tarehe… /7**/2022 mwisho wa kuripoti ni …/07/2022** katika siku hiyo utatakiwa kufika shuleni na kujiandikisha tayari kwa masomo. Wakati wa kujiandikisha utatakiwa kulipa ada ya shule na michango mingine yote na kuthibitisha kuwa umetimiza masharti mengine yote kama inavyoonyesha katika barua hii.

Jaza fomu zote zilizoambatanishwa na uje nazo na kukabidhi wakati wa kuandikishwa. Masomo yanayofundishwa katika shule hii kwa kidato cha tano ni Elimu ya **Uraia, Kiswahili, Kiingereza, Historia, Jiografia, uchumi** na **Hisabati ambapo tunapata mchepuo wa HGK, HKL, HGL, HGE na EGM,**. Jumla ni masomo saba.

**MAHALI ILIPO NA AINA YA SHULE.**

Kiwele sekondari ipo kijiji cha Mfyome yapata km 25 kutoka Iringa mjini katika njia ya kuelekea pawaga. Unaweza kufika shuleni hapa kwa kupanda magari yanayofanya safari ya **Iringa mjini - Itagutwa au Iringa mjini – Kitapilimwa na Iringa mjini - Mfyome .** Usafiri wa basi kutoka **Iringa** mjini unapatikana katika kituo cha basi cha **STENDI KUU YA ZAMANI** nauli ni shilingi **2000/=** tu au barabarambili kwa usafiri wa bajaji nauli ni 2000/= tu.

Shule hii inapokea **wanafunzi wa kutwa kwa kidato cha I-IV na wanafunzi wa bweni kwa kidato cha tano na sita**.

Tafadhali soma maelezo ya ziada hapa chini.

Karibu sana Kiwele Sekondari, nakutakia safari njema ya kuja hapa.

____________________________

**MALIGA E.J**
**MKUU WA SHULE**
**0623185893**

**A. MAELEZO MUHIMU KUHUSU SHULE.**

**MAHITAJI MUHIMU YA SHULE KWA WANAFUNZI WOTE:**

A. Karo /ada ya shule ni Tshs. 70,000/= kwa mwaka au Tshs. 35,000/= kwa muhula.
B. Fedha za tahadhari (caution money) Tshs. 5,000/= na inalipwa mara moja tu.
C. Kitambulisho na picha Tshs. 6,000/=
D. Daftari kubwa (counter books) kumi (10)
E. Mfagio brush ya kusafishia masink ya choo 01 na hardbloom mmoja yenye mpini.
F. Mfagio wa chelewa mmoja (01)
G. Jembe 01 lenye mpini, kwanja 01.( ***vinapatina maeneo ya karibu na shule)***
H. Ndoo moja (01) ya ujazo wa lita 20
I. Ream moja (02) za karatasi (photocopy)
J. Diamond file moja (01) kwa ajili ya mwanafunzi kutunzia kumbukumbu zake.
K. Kalamu za kutosha
L. Vitabu vya tahasusi husika.
M. Scientific calculator kwa tahasusi za HGE NA EGM.
N. Fedha ya Taaluma Tshs. 20,000/= kwa mwaka
O. Ukarabati wa samani Tsh. 15,000/=
P. Matibabu Tshs. 10,000/= kwa mwaka
Q. Fedha Tshs. 30,000/= kwa ajili ya mpishi, walinzi na vibarua wengine.
R. Tshs 2,000/= nembo ya shule.
S. Mchango kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa bweni 20,000/=
T. Gharama ya umeme Tshs 10,000/=
**U. Nakala ya cheti cha kuzaliwa ni lazima**
**V. Nakala ya result slip**

- **MAHITAJI YA BWENI**.

i. Vyombo vya chakula: sahani, bakuli, kijiko, kikombe na jagi la maji ya

Kunywa

ii. Godoro la sponji (2 ½ x 6) na chandarua

iii. Shuka za rangi ya bluu bahari moja na pink moja na mto (pilo).

iv. Tochi moja (01) ya betri mbili itakayotumika kukiwa na tatizo la umeme.

v. Ndoo moja ya lita 10 kwa matumizi ya mwanafunzi mwenyewe.

vi. Nguo za kushindia ni gauni mbili za kijani iliyoiva( ***inapatikana shuleni***)

vii. Neti na Blanketi

viii. Taulo la kuogea, sabuni za kuogea na kufulia na dawa ya meno.

**NB: FEDHA ZOTE ZA ADA NA MICHANGO MINGINE ZIINGIZWE KWENYE**

**ACCOUNT NA.60510015230- NMB - KIWELE SEKONDARI**

**B. SARE YA SHULE**.

i. Shati mbili (02) nyeupe mikono mirefu zisizo na urembo wowote ule.

ii. Sketi mbili (02) za kaki zenye linda box na ziwe ndefu zenye kitambaa kizito kitambaa namba 1024 ***inapatikana shuleni***)

iii. Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili (02) vinavyopigwa rangi.

iv. Soksi nyeupe jozi mbili ndefu.

v. Sweta mbili rangi ya bluu, shingo ya 'V'.

NB: - Nywele ni sehemu ya sare ya shule, zinatakiwa ziwe fupi za kuchana, aidha kucha ziwe fupi na safi wakati wote. Hairuhusiwi kuvaa mapambo ya aina yoyote ile shuleni.

**MAHITAJI MENGINE MUHIMU**

- Kila mwanafunzi atatakiwa kuja na nguo za michezo ambazo ni T-Shirt ya

njano na bukta au tshirt la njano na track suit rangi kijani pamoja na raba rangi nyeupe. **.**

**TRACKSUIT IVALIWE WAKATI ANAKUJA SHULE.**

**MAVAZI HAYA YATAVALIWA SIKU ZA MICHEZO TU.**

- Vazi nje ya darasa na wakati wa kazi ni magauni mawili ya kijani kwa wasichana. Gauni lishonwe mshono wowote ila lisiwe la kubana , fupi au kwapa wazi.

- Mwanafunzi haruhusiwi kufanya kazi na sare ya shule ikumbukwe kuwa kazi za mikono ni sehemu ya masomo ya mwanafunzi. Mavazi ya aina nyingine nje ya haya yaliyotajwa hayaruhusiwi kabisa shuleni.

**MWISHO.**

1. Maagizo yote yatakaguliwa siku ya kuripoti. **Mwanafunzi hatapokelewa endapo hatakuwa amekamilisha maagizo yaliyomo ndani ya fomu hii**. Ukifika shuleni utasomewa tena sheria, kanuni na taratibu za shule hii. Ni wajibu wako kutii na kuzifuata kikamilifu. Ukikosea utaonywa kwa maandishi/mdomo au utaonywa kwa kupewa adhabu na ikilazimu utasimamishwa masomo kwa muda (suspension) au kufukuzwa shule kabisa ikibidi kwa mujibu wa sheria.
2. Kwa usikivu na utulivu wa kitaaluma na kwa usalama wa kimalezi kwa mwanafunzi**, "SIMU ZA MKONONI HAZIRUHUSIWI SHULENI"** na mawasiliano yote yanayohusu malezi ya mwanafunzi kati ya mzazi/mlezi na utawala wa shule ni kupitia ofisi ya malezi/makamu mkuu wa shule KWA NAMBA HIZI **0786 88 49 62/ 0624 015691/ 0755 314325/ 0672 739555 zinapatikana**

**kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 11 jioni. Tofauti na hapo wasiliana** mkuu wa shule kwa namba zilizopo ukurasa wa kwanza.

3. Mwanafunzi akikutwa ametumia simu maeneo tofauti na yaliyoanishwa **ATAFUKUZWA SHULE.**
4. Mwisho kabisa nachukua nafasi hii tena kukukaribisha sana hapa Kiwele Sekondari na ni matarajio yangu kuwa ufikapo hapa utatumia vema fursa hii muhimu uliyotunukiwa na taifa lako, kwani wengi wameikosa.

## SHERIA ZA SHULE

Tabia njema ni ya lazima na inatiliwa mkazo hapa shuleni. Mwanafunzi mwenye tabia mbaya hafai kupewa elimu ya sekondari au hata elimu ya juu. Ni lazima mwanafunzi awe na tabia nzuri na kufuata taratibu za shule pia kuwatii wafanyakazi na walimu wengine wenye mamlaka. Heshima na adabu kwa mtu yeyote ni kitu cha lazima.

### SHERIA KWA UJUMLA

1. kunywa pombe, kuvuta sigara/madawa ya kulevya au kiko ni mwiko
2. Uzinifu wa aina yoyote ni kosa kubwa sana na hairuhusiwi shuleni.
3. Kila mwanafunzi ni lazima awe mtiifu kwa walimu wake wote, wafanyakazi wote, viranja wote wa shule, na wakuu wengine wote. Ujeuri na ubishi wa aina yoyote ni mwiko, kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono zote.
4. Matusi ya aina yoyote, yawe ya kusema au kuandika hayaruhusiwi shuleni
5. Kila mwanafunzi lazima aheshimu na kutunza mali ya shule, uharibifu wowote utakaotokea itabidi ugharimiwe na mwanafunzi mwenyewe.
6. Sare za shule (uniform) ni lazima zivaliwe wakati wote wa masomo.
7. Wizi wowote hauruhusiwi shuleni, iwe ni mali ya shule au mali ya mwanafunzi au mfanyakazi.
8. Usafi wa mwili, mavazi, madarasa, viwanja ni wajibu wa kila mwanafunzi.
9. Ugomvi wa kupigana au maneno ni mwiko shuleni.
10. Kuchelewa kwa aina yoyote ni kosa.
11. Tabia njema shuleni na nje ya shule ni wajibu na ni lazima kwa kila mwanafunzi.
12. Taa za shule na maji ya shule ni lazima vitumike kwa uangalifu.
13. Magazeti au vitabu vyenye picha au maneno yasiyofaa havitakiwi shuleni.
14. Upokeaji au uandishi wa maneno yasiyofaa ni mwiko shuleni.
15. Uhusiano wa mwanafunzi wa kike na wa kiume uwe ni wa kimasomo tu na si vinginevyo. Aidha uwe ni ule wa kaka na dada.
16. Unapaswa kufahamu mipaka ya shule na kutotoka nje bila ruhusa.
17. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mwalimu au mfanyakazi yoyote isipokuwa inapolazimu kwa ruhusa maalumu. Maeneo hayo ni nje ya mipaka ya shule.
18. Si ruhusa kutoka katika nje ya eneo la shule wakati wa masomo bila ruhusa au pass.
19. Hairuhusiwi kugoma, kusababisha mgomo hapa shuleni.
20. Mwanafunzi hairuhusiwi kuwa na mimba, kutoa mimba au kusababisha mimba kwa mwenzake au kwa mtu mwingine yeyote.
21. Lugha ya mawasiliano hapa shuleni ni kiingereza. Ni lazima kila mwanafunzi kutumia lugha hiyo wakati wote awapo hapa shuleni.

**SHERIA ZA MADARASANI**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi shule siku zote za masomo.
2. Kila mwanafunzi anahitajika kuhudhuria vipindi vyote vya masomo bila kukosa.
3. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria siku zote za masomo bila kukosa iwapo dharura yoyote itatokea mzazi au mlezi atoe taarifa mapema kwa uongozi wa shule.
4. Darasani ni mahali pa kujifunza, kelele ya aina yoyote darasani hairuhusiwi. Kila mwanafunzi anatakiwa kukaa kufuata mpango uliowekwa na mwalimu wa darasa
5. Katika madarasa, wanafunzi hawana ruhusa ya kukalia viti au meza za walimu
6. Kila darasa limegawiwa eneo la kazi (class areas) kila mwanafunzi itabidi ashiriki kikamilifu kufanya usafi kwenye eneo hilo.

**MAHUDHURIO:**

Kuthamini muda na kuwepo mahali unapotakiwa kwa wakati na kwa mjibu wa ratiba

1. Kuwahi kuamka na kufanya usafi katika eneo lako na kufika mapema mstarini kwa kadili ya mahitaji ya siku.
2. Kuwepo shuleni na kuhudhuria masomo yote na vipindi vyote darasani na nje ya darasa mfano Baraza, Umoja wa masomo, Vikao vya madarasa na hostel (Bweni) na vikundi vinavyo tambulika kisheria, dini na kufanya kazi zote za mikono.

**HESHIMA:**

i. Kuwakarimu, kuwathamini na kuwaheshimu

a.Wanafunzi wenzako wote b. Wakubwa wako na walezi (mzazi, walimu, wanajamii).

ii. Kusimama na kusalimu, kupokea wanaokuzidi kiumri wanapoingia au kupita ulipo bila kujali jinsia yao.

iii. Kutumia lugha nzuri wakati wowote na mahali popote nje na ndani ya shule

iv. kusaidiana na kushirikiana na wanafunzi wengine katika kazi mbalimbali

v. Kuheshimu na kuthamini kazi za aina zote halali, kuheshimu taratibu za mikutano, ofisi za shule na mali za Umma.

vi. Kuheshimu bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa serikali na Nembo ya Taifa.

vii. Kukaa kimya darasani na kutoka kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo darasani.

ix. Baadhi ya tabia ambazo haziruhusiwi kwa mwanafunzi.

- Kuvuta sigara, madawa ya kulevya na pombe.
- Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu/uchafu
- Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima au yasiyokubalika au kubana mwili.
- Kugombana, kupigana, kutukana na kudharauliana.
- Uasherati, wizi, utapeli, ulaghai na mengineyo yanayofanana nayo.

**MIPAKA YA SHULE:**

i. Unapaswa kufahamu na kuelewa vizuri mipaka ya shule na usitoke ndani ya mipaka hiyo bila ruhusa/kibali maalumu baada ya kufika shule.

Ii Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila ruhusa

a. Ofisi ya walimu na maabala.

b. nyumba za walimu au watumishi wasio walimu

iii. Hairuhusiwi kabisa kwa mwanafunzi kutembelea

a. Vilabu vya pombe na baa
b. Majumba ya starehe
c. Majumba ya kufikia wageni
d. Madanguro.

**SARE:**

Unatakiwa kuvaa sare za shule kwa mshono uliokubaliwa na kwa wakati kama taratibu za shule zinavyoelekeza hasa.

1. Wakati wa masomo darasani
2. Safari zote za nje ya shule
3. Wakati wa kwenda Hospitali
4. Wakati wa maandamano.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE NI:**

1. Wizi, Uasherati, Ubakaji na Ushoga, Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya, Uvutaji wa bangi.
2. Makosa ya jinai kadiri ya sheria za nchi, kupiga au kupigana.
3. Kuharibu mali kwa makusudi, Kudharau Bendera ya Taifa.
4. Kuowa au kuolewa, kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
5. Kutoa mimba, kugoma kuchochea na kuongoza matendo ambayo yanavuruga amani na usalama wa watu.

6. Kukataa adhabu kwa makusudi, kutohudhuria masomo darasani kwa mujibu wa sheria.
7. Kugoma na kuhamasisha mgomo
8. Kutoa lugha ya matusi kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla
9. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika maeneo ya shule.(***kabla ya kufukuzwa shule mwanafunzi,mzazi/mlezi atatakiwa kulipa gharama za uharibifu wa miundombinu ya shule***

**MATIBABU:**

Wagonjwa wote watapata matibabu ama huduma ya kwanza shuleni ikishindikana kupata huduma ya matibabu yanayohitajika, basi muuguzi atamshauri mwalimu wa zamu/idara ya malezi ambaye ataandika ruhusa ya kwenda kutibiwa nje ya shule.

**USAFI**

Usafi ni sehemu ya haiba. Hivyo usafi ni wajibu wa kila mwanafunzi kama sehemu muhimu ya wajibu wa kila siku utazingatia yafuatayo:

i. Usafi binafsi wa mwili na mavazi yako.

Ii Usafi wa maeneo mbalimbali ya shule kama utakavyopangiwa mfano ukumbi

wa chakula, vyoo, madarasa na maeneo ya shule n.k

iii. Vyakula viliwe ndani ya bwalo la chakula tu au sehemu iliyopangwa tu. Ni kosa kupeleka chakula bwenini.

**MATUMIZI NA UTUNZAJI WA MALI ZA SHULE NA MAZINGIRA**

I. kila mwanafunzi atatakiwa kutumia na kutunza vizuri mazingira na mali za shule kama vili majengo, viti, meza, madawati, majembe, vitabu, vitanda, ndoo na vifaa vyote vya shule.

II. Hakikisha taa zote zimezimwa wakati wa mchana na funga mabomba ya maji ukiyakuta wazi.

III. Weka mazingira ya shule kuwa safi na kuvutia kwa kutunza miti, kuokota karatasi na uchafu wowote. Pita kwenye njia za miguu kama unavyoelekezwa na sheria za shule. Usikatishe katika viunga na kukanyaga maua na majani yaliyooteshwa.

**MAWASILIANO**

Mawasiliano ya ana kwa ana na uongozi wa shule ni muhimu sana kwa maendeleo ya mwanao. Kama litatokea tatizo lolote linalomuhusu mwanao kimasomo au kitabia ni vizuri mzazi uwasiliane na uongozi wa shule mara moja. Pia shule itawasiliana nawe mara moja endapo itatokea lazima hiyo. **NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI KUMILIKI SIMU YA MKONONI/ LINE AU KIFAA CHOCHOTE KINACHOHUSIANA NA SIMU AKIWA HAPA SHULENI.**

## ORODHA YA VITABU AMBAVYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NAVYO KULINGANA NA TAHASUSI YAKE

**VITABU VYA HISTORY:**

1. How Europe underdeveloped Africa by Walter Rodney.
2. Africa since 1800, 4th edition by Roland Olive and Atmore.
3. The political economy, imperialism by Nabudere.
4. Mastering Advanced level History book II by Kato.
5. World History Advanced Level by Samweli Mhajida.
6. Focus on modern world History History Advanced Level by Chakupewa.J etal (2012) paper I na Paper II.
7. Contemporary history events volume one first edition by Shibitali C.K
8. Major Events in the World History paper 2 Advanced Level Gervas.M Zombwe.

**VITABU VYA UCHUMI:**

1. Economic simplified East Africa Edition by N.A Saleem.
2. Ambilikile Advanced economic paper I.

**VITABU VYA GEOGRAPHY;**

1. Bunnett (2006) physical geography in diagram for Africa Longman Limited china.
2. Economic geography by Mogarn.
3. Human and economic geography by D.T Msabila.
4. The essential of practical geography Advanced level by Joseph William Njiku (2005).
5. Certificate of Human and economic Geography. By Morgan and Leong Chang.

**VITABU VYA KISWAHILI**

**A. USHAIRI:**

1. Kimbunga - G.Gora (Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili) 1999.
2. chungu Tamu-T.A Mvungu (Tanzania published house) 1985.
3. Mapenzi bora-S.Robert (Mkuki na Nyota) 2003.
4. Fungate ya Uhuru M.S Khatibu.

**B. RIWAYA;**

1. Vuta n'Kuvute- A.Shafi (Mkuki na Nyota)-1999.
2. Kufikilika S.Robert-2003
3. Mfadhili –Hussein Tuwa.
4. Usiku utakapokwisha-Mbunda Msokile-2007

**C. TAMTHILIA;**

1. Moran -E.Mbogo
2. Kivuli Kinaishi –Said Mohamed-2007.
3. Kwenye Ukingo wa Thim-E.Ussein
4. Nguzo Mama-1982.

**ENLISH LANGUAGE**

1. New advanced level English by Charles. E
2. Advanced level English, A practical approach by Nicholous Asheli.
3. Advanced level literature by Nyambari Nyangwine.
4. Advanced level Learners Dictionary.
5. Teaching English as a foreign language by G.Broughton.
6. English form V and VII by M. Kadege.
7. Contempory English for advanced level by Francis Mnyawe.
8. Complete course by M.Kadege.

**B-NOVEL:**

1. The beautiful ones are not yet born by A.K Amah.
2. A man of the people by C.Achebe.
3. Divine providence –Mkuki na Nyota.
4. Encounters from Africa –Macmillan.
5. The rape of the peal-Macmillan.

C**-PLAYS/DRAMA;**

1. An Enemy of the people –H.Ibsen.
2. I Will Marry When I want-EAEP
3. Rwanda Magere by Okoti Omtatah-1991
4. The Pride –EAEP
5. Black Mamba-EAEP.

C**-POETRY;**

1. Selected poem from institute of education.
2. The wonderful Surgeon and other poem-Mkuki na Nyota.

**PURE MATHEMATICS;**

1. Pure mathematics I and II by J, K Backhouse.
2. Advanced level pure mathematics by Kinunda.
3. Advanced level pure mathematics by C.J Tranter- 2006
4. S.Chand mathematics for class XI, volume I and II by H.K DASS R.VERMA 2013
5. Calculator Casio.

**BASIC APPLIED MATHEMATICS (BAM):**

1. Basic applied mathematics for Advanced school form V and VI by Septine

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
SHULE YA SEKONDARI KIWELE

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA TANO**

**SEHEMU YA KWANZA**
(Sehemu hii ijazwe na Mwanafunzi mwenyewe)

Picha

1. Mimi ------------------------------------------------ (Mwanafunzi) kwa hiari yangu nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha Kwanza/Tano katika sekondari ya Kiwele.
   Jina la Mwanafunzi -----------------------------------------------------
   Sahihi ya mwanafunzi------------------------
   Tarehe ----/------/20---
2. Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi
   Mimi ----------------------------------------------------- Mzazi/Mlezi wa ------------------------
   Nakubali/Sikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda awapo shuleni atalazimika kuwa mtii kwa Walimu, Wazazi, Viongozi na Jamii kwa ujumla. Atalazimika kufuata sheria zote za shule. Naahidi kuwa mwanangu atazifuata taratibu zote za shule hadi atakapo maliza shule.

   Jina la Mzazi/ Mlezi ---------------------------------------------------------

   Sahihi ---------------------------
   Tarehe ----/----/20-----

   Namba ya simu……………………………………………

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOANA SERIKALI ZA MITAA**

**KIWELE SEKONDARI**

**FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULE**

**HABARI ZA MZAZI/MLEZI**

**(Fomu hii ijazwe na mzazi/ mlezi iambatanishwe picha ya mzazi /mlezi atayekuwa anawasiliana na walimu shuleni**)

1. Jina kamili la baba ……………………………………………
2. Uraia ………………………
3. Kazi yake ……………………………………………..
4. Namba ya simu……………………………………
5. Jina kamili la mama …………………………………..
6. Uraia ……………………….
7. Kazi yake ……………………………………………………
8. Namba ya simu……………………………………………..
9. Jina kamili la mlezi (iwapo haishi na wazazi wake)……………………………………………………………
10. Namba ya simu ……………………………………
11. Mtoto anaishi na (1) Baba tu (2) Mama tu (3) Wazazi wote (4) mlezi (kata yasiyohusika).
12. Dini ya mzazi/mlezi ……………………………………………………
13. Dhehebu unalotaka mwanao alelewe …………………………..
14. Anuani kamili ya sehemu ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo…………………………………………………………………………………………………………… ………………………………………………
15. Mimi…………………………………………….Mzazi/mlezi wa …………………………………….. nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi. Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri mchapa kazi, na mwenye bidii.

…………………………..                    ……………………………..

Sahihi ya mzazi/mlezi.                    Tarehe

**MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING**

**KIWELE SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**(To be completed by medical officer in suspect of all new students)**

Full name ………………………………………………………………..

Age ……………………..

1. Blood count (red and white) ………………………………………..
2. Urine examination ……………………………………………… ….
3. Stool examination …………………………………………………...
4. Syphilis test …………………………………………………………..
5. T.B test ………………………………………………………………
6. Ear test ……………………………………………………………...
7. Eye test ……………………………………………………………..
8. Spleen ……………………………………………………………....
9. Abdomen ………………………………………………………….....
10. Addition information or any other physical, mental, hereditary of infectious diseases.

    ………………………………………………………………………………………………………………

    ……………………………………………

Treatment after examination.

………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………….

**<u>MEDICAL CERTIFICATE</u>**.

I certificate that the above concerned has been examined and found fit into pursue for further education.

Signature ……………………………..

Designation …………………………..

Station ……………………………….

(Official Stamp) ………………………..

Date …………………………………..

**NB**: Fomu hii ijazwe na Mganga katika hospitali inayotambulika Serikalini.

KIAMBATISHO 01



Rangi na aina ya track suit inayotakiwa ni hiyo iliyo ambatanishwa hapo juu**. ivaliwe wakati anakuja shule.**